**KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA**
**DAYOSISI YA KASKAZINI MAGHARIBI**
**CHUO CHA MAFUNZO YA KILIMO NA MIFUGO IGABIRO**
**S.L.P 212-MULEBA , KAGERA.**
**Simu: 0768733010 (Mkuu wa chuo), 0626456452 (Afisa udahili) au 0757749679**
Baruapepe:igabirotia@gmail.com Tovuti: www.igabirotia.ac.tz

Tarehe: ………………..

Bw/Bi: ………………………………………………..

**YAH: BARUA YA WITO (JOINING INSTRUCTION) KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA KILIMO NGAZI YA CHETI (ASTASHAHADA) MWAKA WA MASOMO 2024/2025 KATIKA MKUPUO WA MWEZI MACHI (MARCH INTAKE)**

**1.0 Utangulizi**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya kilimo ngazi ya cheti (AStashahada)-Certificate in Agriculture Production Course 2023. Nakupongeza kwa kuwa miongoni mwa wachache waliochaguliwa kati ya wengi walioomba. Baada ya kumaliza mafunzo yako utapata elimu ya kutosha ya nadharia na vitendo katika kilimo na baadae kuajiriwa na sekta za umma, binafsi, kujiajiri au kujiunga na chuo kikuu.

Chuo kinamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)-Dayosisi ya Kaskazini Magharibi. Chuo kimesajiliwa na Balaza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) tangu mwaka 2014 na namba yake ya usajili ni (**Cert.No**.**REG/ANE/018**.). Aidha chuo kina ithibati (**Accreditation**).

**Tutaanza kupokea wanfunzi kuanzia tarehe 25 Machi 2024 hadi tarehe 31 Machi 2024 na masomo yataanza rasmi tarehe 3 Aprili, 2024.**

Chuo kinapokea wanachuo wa **kutwa** na **bweni**.

**WANACHUO WA KUTWA**

Gharama za mafunzo kwa mwaka ni shilingi Milioni moja na laki mbili tu (**1,200,000/=),** ambazo utazilipa kwa awamu nne kwa mwaka. Na mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

1. Malipo wakati wa kuripoti chuoni ni **Tsh 300,000/=**
2. Malipo awamu ya pili (Disemba) ni **Tsh 300,000/=**
3. Malipo awamu ya tatu (February) ni **Tsh 300,000/=**
4. Malipo awamu ya nne (Aprili) ni **Tsh 300,000/=**

**WANACHUO WA BWENI**

Gharama za **MAFUNZO**, **MALAZI**, **CHAKULA** na **INTERNET** kwa mwaka ni Milioni moja na laki sita tu **(1,600,000/=),** ambazo utazilipa kwa awamu nne kama ifuatavyo:-

1. Malipo wakati wa kuripoti chuoni ni **Tsh 400,000/=**
2. Malipo awamu ya pili (Disemba) ni **Tsh 400,000/=**
3. Malipo awamu ya tatu (Februari) ni **Tsh 400,000/=**
4. Malipo awamu ya nne (Aprili) ni **Tsh 400,000/=**

**NB**: **Vifaa na michango inayohitajika wakati wa usajili wa mwanachuo wa kutwa au bweni mara afikapo chuoni ni kama ifuatavyo;**

**(KWA WANAFUNZI WOTE)**

i. Ream paper mbili (2) A4 (kwa mwaka)
ii. Cheti cha daktari (Medical certificate of fitness) fomu imeambatanishwa.
iii. Fedha kiasi cha Tsh **20,000/=** kwa ajili ya kulipia T-shirt inayotumika wakati wa matukio muhimu uwapo chuoni (Inapatikana chuoni), **pesa hii inalipwa chuoni kwa mhasibu.**
iv. Kikokotozi (Scientific calculator) – 35,000/= (inapatikana chuoni)
v. Ovalori – 30,000/= (inapatikana chuoni)
vi. Gambuti – 15,000/= (inapatikana chuoni)
vii. Vitendea kazi **(Tsh 15,000/=)**
viii. Vifaa vya usafi **(Tsh 10,000/=)**
ix. Fedha ya uthibiti ubora (Quality Assurance) – 15,000/=
x. Fedha kwaajili ya tahadhari (Caution Fee) **(Tsh10,000/=)**

**KWA WANACHUO WA BWENI**

**LAZIMA mwanchuo aripoti na mahitaji yafuatayo;**

- - Mwanachuo anatakiwa kuja na godoro 2.5`x 6`, shuka mbili, blanket, sweta / jaketi, taulo, chandarua, mto, ndoo/beseni, miswaki, sabuni, mafuta ya kupakaa, sahani, bakuli, vijiko, kikombe na vifaa vinginevyo vya usafi binafsi.

**N.B Tafadhali** lipa michango yote kwenye akaunti tajwa hapo chini kwani hatupokei pesa tasilimu, isipokuwa risiti ya benki (Bank pay in receipt)

**Namba ya akaunti: 0150216227000**
**Jina la akaunti (CRDB Bank) – ELCT IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICULTURE**


**Mahali chuo kilipo:**

- Chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo Igabiro kipo wilayani Muleba – Kagera. Kutoka Muleba mjini ni Kilometa 15 magharibi ukipitia barabara ya Nshamba. Na kutoka Nshamba kufika chuoni ni kilometa 3 kusini mwa Nshamba barabara ya kwenda Kabale upande wa kushoto kuna kibao kinachoonesha chuo kilipo. Kutoka manisipaa ya Bukoba, pita barabara ya Bukoba – Muleba au Bukoba – Kamachumu kuja Nshamba. Mara ufikapo chuoni, wasiliana na afisa udahili (Admission Officer) kwa usajili na malazi pamoja na huduma zingine muhimu.
- Hakikisha unakuja na fomu ya kujiunga na chuo (joining instruction) wakati wa usajili.
- Unatakiwa kuripoti chuoni mapema kama tarehe zinavyo elekeza, kushindwa kufanya hivyo inaweza kupelekea kupoteza nafasi hiyo.

**Maelekezo ya jumla**

- Masomo yako yatachukua muda wa miaka miwili kwa ngazi ya Certificate (Astashahada) na mwaka mmoja kwa ngazi ya Diploma (Upgrading)
- Lipa ada na michango mingine kwa wakati sahihi ili kuepusha usumbufu kwa Mwanachuo na upande wa utawala.
- Mwanchuo awapo chuoni ni lazima kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na chuo ili kuepusha usumbufu.

**“Kwa niaba ya watendakazi, wanachuo na jumuiya nzima ya chuo tunakutakia safari njema na mafanikio katika masomo yako, karibu Igabiro”.**



……………………

Sadock Stephano

**Mkuu wa Chuo**




## KARIBU SANA CHUONI KWETU

**EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA**
**NORTH WERSTEN DIOCESE**
**IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICUTURE**

**P. O.BOX 212-MULEBA,**
**Mobile Phone: 0685807180 (Principal)/0625960073/0626456452 (Admission officer)**
**Email:** igabirotia@yahoo.com and **Website:** www.igabirotia.ac.tz

TO: The Medical Officer

…………………………………………

…………………………………………

1. Name………………………………………………………………………………..
2. Age ………………………………………………………………………………..
3. Weight ……..………………………………………………………………………
4. Blood Examination: Hemoglobin ……………………………………………………

   Any abnormalities noted ………………………………………………….................
5. Stool Examination……………………………………………………………………
6. Urinalysis………………………………………………………………………………
7. T.B. Test (if negative, was immunization given)

   ………………………………………………………………………………………
8. Eyes ………………………………………………………………………………..
9. Chest……………………………………………………………………………………
10. Abdominal Examination …………………………….………………………….........
11. Spleen ……………………………………………………………………………

    Liver ………………………………….………………………………………………
12. Any clinic complaints not noted above ………………………………………….

    Asthma ………………………………………………………………………………

    Headache ……………………………………………………………………………

Signature and stamp

(**Medical Officer)**